656

**MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI**
**(EWURA)**

**MALALAMIKO NAMBA: GA.71/135/CZ/2024/14**
**NAMBA YA LOIS: COMP-2024-00000206**

**KATI YA**

**YONA W. MSHANA ............................................................................ MLALAMIKAJI**

**NA**

**SHIRIKA LA UMEME TANZANIA (TANESCO) ........................... MLALAMIKIWA**

---

**TUZO YA MAKUBALIANO**

---

***(Imetolewa na Kamati ya Sheria na Utawala ya Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA katika kikao chake cha 144 cha tarehe 17 mwezi Januari 2025)***

## 1.0 Maelezo ya Awali

Mnamo tarehe 28 Agosti 2024, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji "EWURA" ("Mamlaka") ilipokea malalamiko kutoka kwa Bw. Yona W. Mshana akiwakilishwa na Bw. Joffrey Y. Mshana wa S. L. P. 7 Mang'ula, Kijiji cha Mwaya "A", Kilombero, Mkoa wa Morogoro (Mlalamikaji) dhidi ya Shirika la Umeme Tanzania ("TANESCO") (Mlalamikiwa). Mlalamikaji analalamikia kitendo cha Mlalamikiwa kumwekea deni bambikizi la Shilingi 9,810,624.02

wakati yeye analifahamu deni la Shilingi 1,300,000/= katika dira yake ya LUKU yenye namba 54151042683.

Mlalamikaji anaendelea kueleza kwamba mwaka 2006, dira yake ya malipo baada ya matumizi iligundulika ina deni la TZS 1,300,000/= na Mlalamikaji alichukua hatua mbalimbali ikiwemo kwenda ofisini ambapo Mlalamikiwa alimbadilishia dira na kuwawekea dira ya malipo kabla (LUKU) na kuwa deni lilianza kulipwa kwa kuwa kila Mlalamikaji anaponunua umeme hukatwa deni hilo.

Mlalamikaji anaeleza kuwa baada ya kuwa anakatwa deni hili kila anunuapo umeme alitegemea deni kupungua, lakini mnamo mwezi Mei 2024 Mlalamikiwa alifika nyumbani kwa Mlalamikaji na kumueleza kuwa anadaiwa deni la TZS 9,810,624.02 na aliamua kufuatilia deni hilo kwa kwenda ofisini kwa Mlalamikiwa lakini hakuweza kupata majibu sahihi kuhusu deni hilo wala hakuna hatua ya utatuzi iliyochukuliwa.

Hatimaye, Mlalamikaji aliwasilisha malalamiko yake kwa Mamlaka na kuomba imuamuru Mlalamikiwa kufanya uchunguzi wa kina ili kubaini usahihi wa deni hilo na pindi itakapobainika kuwa deni hilo sio sahihi, basi lifutwe na pesa zilizokuwa zikikatwa pindi alipokuwa akinunua umeme arudishiwe.

Baada ya kupokea malalamiko ya Bw. Yona W. Mshana tarehe 04 Septemba 2024, Mamlaka (EWURA) ilimwandikia Mlalamikiwa na kumuamuru kuwasilisha utetezi wake kwa maandishi ndani ya siku ishirini na moja (21) kwa mujibu wa Kanuni ya 6 (1) na 7 (1) ya Kanuni za EWURA za Utatuzi wa Migogoro - (EWURA (*Consumer Complaints Settlement Procedure), Rules 2020)*) TS Na..428.2020.

Mnamo tarehe 23 Septemba 2024, Mlalamikiwa alileta utetezi wake na kuieleza Mamlaka kwamba anakiri kupokea malalamiko haya na ameeleza kwamba deni hilo alilowekewa Mlalamikaji kwenye dira yake ni deni sahihi na limetokana na matumizi yake ya umeme wakati anatumia dira ya malipo baada ya matumizi. Mlalamikiwa ameeleza kwamba baada ya kumwekea Mlalamikaji

dira mpya ya malipo kabla ya matumizi deni hilo lilihamishiwa kwenye dira hiyo mpya ili aweze kulilipa kidogo kidogo kila anaponunua umeme.
Hivyo, Mlalamikiwa anaiomba Mamlaka itupilie mbali malalamiko haya kwani halina msingi.

Vikao vya usuluhishi baina ya pande zote mbili vilifanyika tarehe 18/10/2024 na 06/01/2025 katika ukumbi wa Mountain Peak Hotel uliopo Kilombero, Mkoa wa Morogoro.

Mwisho wa kikao cha usuluhishi tarehe 06/01/2025, muafaka ulifikiwa kwa makubaliano yafuatayo:-

(i) Kwamba Mlalamikaji atalipa deni la TZS 759,697.77/= badala ya deni la TZS 9,810,624.02/= ambazo alikuwa akilalamikia awali; na

(ii) Kwamba Mlalamikaji kulipa deni hilo la TZS 759,697.77 ambapo deni hilo litaanzwa kukatwa mwezi Februari 2025 kila anunuapo umeme.

Makubaliano haya yamefupishwa kimaandishi kama inavyoainishwa kwenye Kanuni ya 14 (4) ya Kanuni za Taratibu za Kutatua Migogoro Tangazo la Serikali Na. 428 la 2020 na kama inavyoainishwa kwenye fomu ya makubaliano.

## 2.0 <u>Makubaliano</u>

Pande zote mbili zimefikia muafaka kuwa Mlalamikiwa atalipa deni la TZS 759,697.77/= badala ya deni la TZS 9,810,624.02/= ambazo alikuwa akilalamikia awali na Mlalamikiwa amekubali Mlalamikaji kulipa deni hilo la TZS 759,697.77/= ambapo deni hilo litaanza kukatwa mwezi Februari 2025 kila anunuapo umeme.

Kwa mujibu wa Kanuni ya 14 (5) ya Taratibu za Utatuzi wa Migogoro makubaliano haya yameandikishwa kama Tuzo ya Mamlaka. Kila pande itabeba gharama zake katika shauri hili.

**IMETOLEWA KWA LAKIRI** ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji Dodoma tarehe 17 mwezi Januari 2025.

..............................

**TONI S. MBILINYI**

**KATIBU WA BODI**